



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO



SimuNa:027-2977216/027-297721
Nukushi Na. 027-2977216/027-2977217
Barua pepe :ded@lushotodc.go.tz
Tovuti:www.lushotodc.go.tz
Unapojibu tafadhari taja:

S.L.P. 32,
Lushoto
TANZANIA

Kumb. Na. LDC/L.10/106/19

21/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI
YA MAKAZI NA POSTIKODI HALMASHAURI YA LUSHOTO.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Mitaa na Vitongoji vyote vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

A) SIFA ZA WAOMBAJI

- i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- ii) Awe Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.
- iii) Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iv) Awe anamiliki Simu janja (Smartphone) inayotumia mfumo wa uendeshaji wa android(Android OS) yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima(24hrs).
- v) Awe na barua pepe(email address) na nywila(password) inayofanya kazi.
- vi) Awe na uwezo wa kusoma/kutafsiri ramani za mitaa/Kitongoji.
- vii) Awe ni mkazi wa Kata/Kijiji/Kitongoji husika.

S.L.P 32,Lushoto,Tanga, SimuNa:027-2977216/027-297721,Barua Pepe:ded@lushotodc.go.tz,
Tovuti:www.lushotodc.go.tz

viii) Awe tayari kufanya kazi katika kata yeyote ndani ya Halmashauri ya Lushoto.

ii) KAZI NA MAJUKUMU.

- i) Kugawa/Kuandika namba za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma.
- ii) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma.
- iii) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma kwa kutumia programu tumizi ya mfumo wa anwani za makazi.
- iv) Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.
- v) Muda wa kazi Utazingatia Mkatoba wa kazi.

iii) MAOMBI YA AMBATANISHWE NA ;

- i) Nakala ya cheti cha Kidato cha mte na kuendelea.
- ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii) Picha mbili za Passport size.
- iv) Barua ya maombi ipite kwa Mtendaji wa kijiji na kata anapoishi.

iv) JINSI YA KUTUMA MAOMBI.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu inayopatikana muda wote, pamoja na barua pepe (Email) inayofanya kazi na kuwasilishwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO,

S.L.P 32.

LUSHOTO.

Aidha chini ya Bahasha upande wa kulia iandikwe OAZM/LDC/2022/001.

S.L.P 32, Lushoto, Tanga. Simu Na: 027-2977216/027-297721, Barua Pepe: ded@lushotodc.go.tz,
Tovuti: www.lushotodc.go.tz

E) TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/02/2022 saa 9.30 Alasiri.

..... | *Fernand*

IKUPA HARRISON MWASYOGE

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA

LUSHOTO.

S.L.P 32,Lushoto,Tanga, SimuNa:027-2977216/027-297721,Barua Pepe:ded@lushotodc.go.tz.
Tovuti:www.lushotodc.go.tz